

Abunuwasi alipata wageni kutoka kijijini kwao waliokuja kumzuru. Alikwenda kwa jirani yake aitwaye Kalulu kuazima sufuria kubwa ya kuwaandalia wageni wali wa pilau. Siku ya pili baada ya wageni kuondoka, Abunuwasi aliirudisha ile sufuria pamoja na kijisufuria kidogo ndani yake. Kalulu alishtuka na kumwuliza, “Mbona umerudisha chombo changu pamoja na hiki kijisufuria kidogo?”

“Usishtuke jirani yangu Kalulu. Hii sufuria yako kubwa ndiyo iliyozaa hiki kijisufuria kidogo,” Abunuwasi alijibu na huku anatabasamu. Abunuwasi aliendelea kukariri kuwa kile kijisufuria kidogo si chake, bali kilikuwa kimezaliwa na ile sufuria kubwa. Mwishowe Kalulu alisadiki kuwa kile kijisufuria kidogo ni mtoto wa ile sufuria yake na akazipokea sufuria zote mbili kwa furaha.

Wiki ya pili, Abunuwasi alirudi tena kwa Kalulu kuazima sufuria.

“Nyumba yangu haikosi wageni siku hizi,” Abunuwasi alitamka huku akitabasamu.

“Lakini mimi nakuona wewe tu, siwaoni hao wageni wako,” Kalulu alitamka.

“Wametoka kwenda sokoni,” Abunuwasi alijibu harakaharaka, “ni wageni wengi na watakaa kwangu kwa muda wa siku tatu,” Abunuwasi akaongeza.

“Kwani unahitaji tena sufuria?” Kalulu aliuliza.

“Ndiyo, jirani. Tena nahitaji sufuria nyingi tafadhali,” Abunuwasi alijibu.

Kalulu aliingia jikoni akaleta sufuria zote alizokuwa nazo. Alitoa vile vile kile kijisufuria kidogo kilicholetwa na Abunuwasi. Alikuwa na tamaa ya kujipatia sufuria zaidi zitakazozaliwa.

“Nitakurudishia sufuria zote wiki ijayo, baada ya wageni kuondoka,” Abunuwasi alimwambia jirani yake.

Kalulu alisubiri zaidi ya wiki mbili kumngoja Abunuwasi arudishe sufuria zake pamoja na vijisufuria vidogo vidogo vitakavyozaliwa. Wasiwasi wake ulipozidi alitoka kwenda kumfuatia Abunuwasi nyumbani kwake. Alibisha mlangoni na alipoingia ndani alishtuka kumwona Abunuwasi akilia. Alipomwuliza sababu za kulia, Abunuwasi alijibu kwa huzuni kuwa sufuria zote alizoazima zimekufa.

“Ama wewe ni juha mkubwa kabisa! Sufuria zitawezaje kufa!” Kalulu alifoka.

“Juha ni wewe!” Abunuwasi alijibu kwa ukali.



“Kwa nini unaweza kuamini kuwa sufuria inaweza kuzaa na usiamini kuwa vile vile inaweza kufa!”

Majirani walifika waliposikia mabishano baina ya Kalulu na Abunuwasi. Kalulu alieleza mambo yalivyokwenda tangu mwanzo mpaka mwisho. Watu walicheka mpaka mbavu zikawauma.

Msamiati

kumzuru	:	kumtembelea.
kuwaandalia	:	kuwatayarishia.
kukariri	:	kurudia tena maneno hayo hayo.
tamaa	:	hamu kubwa ya kupata jambo.
alifoka	:	alisema kwa ukali.
mabishano	:	magombano; utesi.

A. Ufahamu

I. Jibu maswali haya

- Wageni aliopata Abunuwasi walitoka wapi?
- Abunuwasi alitafuta msaada gani wageni walipofika mara ya kwanza?
- Abunuwasi alitoa sababu gani alipompa Kalulu kijisufuria kidogo?
- Kwa nini Kalulu mara ya pili alimwazima Abunuwasi sufuria zake zote?
- Kati ya methali hizi, ni methali gani ambayo haihusiki na hadithi ya Abunuwasi?
 - Mwiba wa kujichoma hauambiwi pole.
 - Wajinga ndio waliwao.
 - Tamaa mbele, mauti nyuma.
 - Paka akiondoka panya hutawala.
 - Akili nyingi huondoa maarifa.